# Hatima ya Maisha ya Waafrika katika Bunilizi za Kiswahili: Mwegamo wa Kifalsafa

Martina Duwe
Chuo Kikuu Mzumbe
*magriccola@gmail.com*

**Ikisiri**
Makala hii imefafanua sababu za hatima ya maisha ya mwanadamu kulingana na fikra za Waafrika kwa kurejelea riwaya za *Utengano* (1980) na *Tata za Asumini* (1990). Data za msingi zilizofafanuliwa katika makala hii zimepatikana maktabani kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Nadharia ya Udhanaishi imetumika kama mwegamo muhimu katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika katika utafiti uliofanyika. Matokeo yanaonesha kuwa utajiri wa maarifa yaliyomo ndani riwaya teule husawiri maudhui na fikra halisi za Waafrika kulingana na tamaduni zao. Fikra hizo hudhihirisha falsafa inayotawala maisha yao. Pia, hubainisha sababu mbalimbali za hatima ya mwanadamu kulingana na mitazamo ya Waafrika. Kifo ni miongoni mwa sababu zilizobainika wazi katika riwaya teule kuwa kinasababishwa na maamuzi ya Mungu, maovu ya mwanadamu mwenyewe na watu wanaomzunguka katika mazingira yake halisi; na namna Waafrika wanavyofikiri juu ya sababu za hatima ya maisha yao. Mwandishi anayaonesha haya ili kudhihirisha uhalisi wa fikra za jamii yake kama sampuli ya jamii za Kiafrika. Makala hii inahitimisha kuwa fasihi andishi inahifadhi na kuonesha maarifa yanayoisawiri jamii husika.

**Dhana Muhimu:** Falsafa, Fasihi, Hatima, Kifo na Mitazamo ya Waafrika kuhusu sababu za hatima ya maisha yao.

## Utangulizi

Falsafa ni taaluma inayojihusisha na uchunguzi na ufafanuzi wa mitazamo ya watu ili kubaini ukweli unaozingatiwa katika kuendesha maisha yao ya kila siku (Duwe, 2016 & Wamitila, 2016). ivyo, tunapozungumzia falsafa tunarejelea kanuni na taratibu zinazofungamana na misingi ya tamaduni za jamii husika. Kuna uhusiano mkubwa kati ya falsafa na fasihi ya jamii. Kwa jumla, fasihi ya jamii hubeba mitazamo yao katika kuyamulika masuala mbalimbali kulingana na misingi ya tamaduni zao (Simiyu, 2011). Mwandishi wa kazi ya fasihi, dhima yake kuu ni kubainisha masuala mbalimbali ya kimtazamo kwa kurejelea maisha halisi ya jamii yake. Hali hii hutokana na uzoefu wa kimaisha unaomsaidia kupembua kweli mbalimbali za jamii hiyo. Kwa jumla, fasihi ina dhima ya kifalsafa kwa msingi kwamba hutumika kama chombo cha kuhifadhi na kuenezea ukweli juu ya vipengele mbalimbali vya maisha ya jamii (Ponera, 2014). Moja ya kweli zinazozingatiwa na kuthaminiwa na mwanadamu katika mazingira yake ni kuhusu hatima ya maisha yake.

Hatima ni dhana inayorejea ukomo wa jambo fulani. Katika andiko hili tunaitazama dhana hii kwa kuihusisha na mwisho wa maisha ya mwanadamu katika ulimwengu wake halisi. Mwisho wa uhai wa mwanadamu hukamilishwa na tendo la kufa. Kifo ni tukio au tendo la kufikia mwisho wa uhai (TUKI, 2014). Mwanadamu tangu anapozaliwa anakuwa katika safari ambayo huhitimishwa na kifo chake. Kimsingi, hatima ya mwanadamu ni tofauti na hatima ya viumbe hai wengine kwa sababu ndicho kiumbe pekee chenye fikra na utashi juu ya maamuzi ya masuala mbalimbali yanayofungamana na jambo hilo (Godin, 1972 & Shields, 2008). Suala la hatima ya mwanadamu linaweza kutazamwa na kushughulikiwa katika miktadha mbalimbali, hasa ya kisayansi, kihistoria na kifalsafa. Katika makala hii, tunaishughulikia dhana hii kwa kurejelea muktadha wa kifalsafa. Waafrika wana mitazamo mbalimbali inayothibitisha thamani ya maisha yao ikiwamo namna ya kuiendea hatima ya maisha yao. Kwao, suala la hatima ya maisha ya mwanadamu hutazamwa na kuendeshwa kulingana na namna jamii inavyoamini juu ya jambo hilo (Mbiti, 1990). Kuamini huko kunakitwa katika misingi ya kiimani inayozingatiwa katika jamii husika.

Waafrika kiasili huamini kuwa kuna siku mbili ambazo ni muhimu katika uwapo wa historia yao ulimwenguni. Siku hizo ni siku ya kuzaliwa ambapo historia ya mwanadamu huanza na siku ya kufa ambayo huhitimishwa historia hiyo (Baloyi, 2008). Katika suala la kifo, huamini kwamba, kifo chochote cha mwanadamu huwa kina sababu ya kutokea kwake. Fikra hizi zilianza sambamba na mwanzo wa maisha ya mwanadamu ambapo kila jamii ililitazama tukio hilo kwa kuhusisha na sababu zilizodhaniwa kuwa ni za msingi kulingana na tamaduni za imani zao (Idowu, 1973). Baadhi ya sababu za hatima ya mwanadamu kulingana na fikra zao, kwanza, kifo ni maamuzi ya Mungu ambaye alimuumba mwanadamu huyo. Hali hii hutokana na kuamini kwao katika Mungu kama sababu ya chanzo na mwisho wa maisha ya mwanadamu. Pili, Waafrika huamini kwamba watu waliopo katika mazingira anayoishi mwanadamu wanaweza kuwa sababu ya hatima ya maisha ya mwingine kutokana na matendo maovu yadhihirikayo na yasiyodhihirika bayana. Hata hivyo, sababu inayotazamwa zaidi ni ile inayohusishwa na nguvu za kisihiri walizonazo watu hao. Tatu, mwanadamu anaweza kujisababishia hatima yake mwenyewe kutokana na kutenda matendo yanayokinzana na misingi ya tamaduni za jamii yake (Temples, 1959; Makame, 2016 & Mbiti, 2011). Kazi mbalimbali za kibunilizi hususani za Kiswahili, zinadodosa mitazamo hiyo. Makala hii inajadili sababu hizo kwa kurejelea riwaya teule za *Utengano* na *Tata za Asumini.*

**Muhtasari wa Riwaya Teule**

*Utengano* ni miongoni mwa riwaya za awali za mwandishi Said Mohamed iliyochapishwa mwaka 1980. Riwaya hii imebeba maarifa mbalimbali ya kifalsafa kulingana na maisha ya Waafrika. Inazungumzia masuala yanayoisawiri jamii ya mwandishi kama sampuli ya jamii za Kiaafrika. Maudhui ya riwaya hii yanaonesha dhiki aliyoipata mama Tamimu na mwanae Maimuna zilizosababishwa na mfumo dume wa mhusika Maksuudi. Maisha ya Maksuudi yanaonekana kutoridhisha familia

na jamii yake kwa jumla kutokana na anasa, ubabe, uonevu na kushindwa kutatua changamoto za jamii yake kama kiongozi. Mwisho, anaaga dunia kwa mateso makali kwa sababu ya kusosa mtu wa kumsaidia kutokana na kuisambaratisha familia yake kwa ubabe. Matendo mabaya ya mwanadamu, humrudia na kuweza kuwa sababu ya maangamizi yake.

Kwa upande mwingine, *Tata za Asumini* ni riwaya iliandikwa mwaka (1990). Riwaya hii inafafanua athari za malezi aliyopewa Asumini na wazazi wake ambayo hayakumsaidia katika kukabiliana na changamoto zilizopo katika ulimwengu wake. Asumini alipoishi nje na wazazi wake, alibadili mavazi yanasitiri kiwiliwili chote hata kisionekane bali uso na viganja vya mikono pekee. Badala yake anavaa nguo za kisasa na kujiingiza katika vitendo vya anasa zikiwamo za kuchezea disko katika kumbi za starehe jambo ambalo ni kinyume na misingi ya malezi aliyolelewa. Maisha ya anasa yakawa sababu ya maangamizi yake kisaikolojia na kimwili kutokana na kushindwa kukabiliana na changamoto zake. Riwaya hizi zinaonesha jinsi maisha ya mwanadamu katika mazingira yake halisi yanavyoweza kuwa sehemu ya matatizo yake yatakayosababisha jamii kuamua tofauti juu yake au kujihukumu mwenyewe. Mwandishi anayaonesha haya katika riwaya hizi ili kuusawiri uhalisi wa maisha ya jamii yake.

**Kiunzi cha Nadharia**

Misingi ya nadharia ya Udhanaishi ndiyo iliyotumika katika kuchunguza na kuzibainisha sababu za hatima ya mwanadamu kulingana na fikra za Waafrika kwa kujiegemeza katika riwaya teule. Wamitila (2002) na Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba, nadharia hii inakadiriwa kuchipuka mnamo mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Mawazo ya mwanafalsafa ya udhanaishi aitwaye Soren Kierkegaard (1813 - 1885) kutoka katika nchi ya Denmark, ndiyo yalisababisha kuibuka kwa nadharia hii. Simiyu (2011) anaitambua dhana hii kwa jina la ‘Utamaushi’ kama falsafa ya watu katika ulimwengu wanamopatikana. Anaendelea kueleza kwamba, nadharia hii ni falsafa inayohusu dhana ya maisha ya mtu katika ulimwengu wake halisi. Camus (1955) anasema kuwa, udhanaishi ni falsafa inayopembua hisi za mwanadamu kuhusu masuala mbalimbali katika maisha yake. Anayatazama maisha ya mwanadamu kama kitu kisichokuwa na thamani kwa sababu hatima yake ni kifo.

Nadharia hii ina mihimili mingi kulingana na fikra za wataalamu walioshughulikia undani wake wakiwamo Camus (1955), Wamitila (2002), Wafula na Njogu (2007) na Simiyu (2011). Mihimili hiyo imejikita katika kuyamulika masuala makuu matatu. Masuala hayo ni maana ya maisha ya mwanadamu, kuwapo au kutokuwapo kwa Mungu na uhusiano uliopo kati ya mwanadamu na Mungu wake kulingana na kaida za jamii ya mwanadamu huyo. Kwa kujiegemeza katika misingi ya nadharia hii, mtafiti amewatazama wahusika wakuu katika riwaya teule kama wenye kukata tamaa kutokana na kutokuwa na uhakika wa maisha. Changamoto zinazowakabili katika jamii yao zinaonekana kuwa sababu ya kufikia hatima yao. Pia, imetumika

katika kufafanua fikra za wahusika hao zilizojiegemeza katika muktadha wa kidhanifu katika kubainisha mazingira ya utokeaji wa kifo cha mwanadamu. Mwegamo huu umefaa katika kuchunguza na kuchanganua sababu za hatima ya maisha ya Waafrika katika riwaya za *Utengano* na *Tata za Asumini*.

**Methodolojia**

Makala hii imefafanua sababu za hatima ya maisha ya mwanadamu kulingana na fikra za Waafrika kwa kurejelea riwaya teule. Matokeo ya makala hii yametokana na uchunguzi uliofanyika katika mwegamo wa kitaamuli. Kimsingi, katika mwegamo huu, mtafiti hutumia tafakuri ya kina katika kuhusisha taarifa mbalimbali zilizopatikana katika utafiti na kutoa ufafanuzi kwa kuzingatia misingi ya nadharia husika pamoja na ithibati bayana (Ponera, 2019). Uchunguzi ulifanyika maktabani ambapo nyaraka mbalimbali zilisomwa na kupata maarifa yaliyomo katika makala hii. Riwaya za *Utengano* na *Tata za Asumini* ziliteuliwa kama nyaraka za msingi katika kuchunguza sababu za hatima ya maisha ya Waafrika kulingana na fikra zao. Uteuzi huo umezingatia kigezo cha utozelevu wake wa maarifa ya kifalsafa yanayoisawiri maisha halisi ya Waafrika.

**Sababu za Hatima ya Maisha kwaWaafrika**

Katika jamii ya Waafrika, kifo kinapotokea kinahusishwa na sababu mbalimbali ambazo kwayo mitazamo yao hubainika. Sababu hizo hutegemea namna na wakati wa utokeaji wa kifo kulingana na tamaduni za jamii husika (Mbiti, 1990). Kuna sababu mbalimbali zinazosababisha hatima ya maisha ya mwanadamu katika riwaya teule kulingana na mitazamo ya Waafrika. Kipengele kinachofuata kinabainisha baadhi ya sababu zilizojitokeza katika riwaya teule zilizochunguzwa katika makala hii.

**Kifo ni Maamuzi ya Mwenyezi Mungu**

Waafrika huamini kwamba, moja ya sababu za hatima ya mwanadamu ni Mungu mwenyewe. Fikra zao zimejikita katika kutazama na kuamini katika Mungu kama asilina sababu ya hatima yao ya maisha katika ulimwengu halisi. Tangu zamani Waafrika walikuwa na dini zao zilizowaaminisha katika Mungu waliomwamini. Maisha yao yalijikita katika kumtegemea Mungu kwa kila jambo kulingana na tamaduni zao za kuamini juu ya jambo hilo (Idowu, 1973). Mungu kwao ndiye mwenye nguvu namwenye maamuzi ya hatima ya maisha ya mwanadamu katika ulimwengu wake halisi (Murphy, 2003). Waafrika huamini kuwa, kifo kwa mwanadamu ni suala linapangwa na Mungu pasipo mwanadamu huyo kufahamu wakati na mahali kitakapotokea kifo chake. Jambo hili ni siri yake pekee na hakuna mwenye uwezo wa kuitambua siku ya hatima yake.

Kwa Waafrika, mwanadamu anapokufa, wafiwa hulia kwa kujiegemeza katika kulihusianisha jambo hilo na maamuzi ya Mungu. Daima husema semi mbalimbali zenye mwegamo huo kama vile ‘Mungu mbona umetufanya tuwe wakiwa, kwa nini umeruhusu haya kutokea, utusaidie kwa maana peke yetu hatuwezi, tupe faraja yako

ee Mungu'. Semi hizi hudhihirisha ya kuwa, Waafrika huhusisha suala la hatima ya maisha ya mwanadamu na nguvu au maamuzi ya Mungu ambayo hayapingiki na mwanadamu yeyote. Endapo Mungu hajapanga hatima ya maisha ya mwanadamu itokee, basi kamwe haitatokea hata kama mwanadamu huyo atapitia changamoto nyingi. Huu ni mtazamo wa kidhanifu ambapo jamii nyingi za Kiafrika hudhani kuna nguvu nyingine inayoweza kuamuru juu ya hatima yao ya maisha. Jambo hili hudhihirisha uhusiano wao na Mungu kama kiumbe kikuu na chenye mamlaka katika uhai wa mwanadamu.

Kazi mbalimbali za kifasihi zinadokeza fikra hizi na kudhihirisha wazi kwamba Mungu kama hajapanga kifo kitokee, kamwe hakitatokea hata kama mwanadamu huyo atapitia katika magumu ya namna gani kama vile ugonjwa wa muda murefu. Mwandishi katika riwaya ya *Utengano*, amesawiri jambo hili kupitia wahusika wake. Haya yanabainika kupitia hali ya ugonjwa wa muda murefu uliomkumba Maksuudi. Mwandishi anafafanua:

> Mbali na yale mengine ya ulimwengu yaliyomkuta na maradhi juu! Anajuta. Huu ulikuwa wakati uliomjulisha Maksuudi kuwa pesa zilitumika na watumishi walitenda waliyoyatenda, lakini kuna mengi yasiyofanyika kwa pesa. Na sasa Maksuudi Mungu amemuafu. Kamuafu si haba angalau anaweza kukokota mguu (Mohamed, 1980:103).

Data hiyo inaeleza kuwa jamii haikufikiria kuwa Maksuudi angeweza kuishi kwa kipindi cha muda mrefu kutokana na ugonjwa aliokuwa nao. Sambamba na hilo, hata yeye mwenyewe hakudhani kama angeweza kuwa hai kutokana na kuugua huko. Pamoja na uwezo wake wa kipesa, bado wanajamii humtazama Mungu kama sababu ya Maksuudi kuendelea kuishi kulingana na hali aliyokuwanayo. Fikra hizi zinaonesha kwamba, Mungu ndiye mwenye maamuzi ya kutokea kwa hatima ya mwanadamu kwa wakati alioupanga. Mawazo haya yanadhihirisha mtazamo wa Waafrika kwa jumla wenye kubainisha kwamba hatima yamwanadamu hupangwa na Mungu kwa kuwa ana maamuzi juu ya jambo hilo kwa kila mwenye uhai.

Sambamba na hilo, Waafrika huamini kwamba mwanadamu anapokufa anakuwa ameitwa na Mungu wake na hivyo, anarudi kwake aliyemuumba (Idowu, 1973). Jambo hili linabainika katika kazi mbalimbali za kibunilizi ili kudhihirisha fikra za Waafrika kwa jumla zinazojiegemeza katika kuamini uwezo wa Mungu kama sababu mojawapo ya kufikia hatima yao. Katika riwaya ya *Utengano*, mwandishi anathibitisha wazi jambo hili kupitia mhusika wake mkuu Maksuudi. Anatueleza kwamba, Bwana Maksuudi alipokuwa mgonjwa sana aliomba dua kwa Mungu wake kila wakati ili asiamuru hatima yake mapema mpaka aione familia yake akiwamo mwanaye mpendwa Maimuna. Mwandishi anasema:

> Na sasa hajui Maimuna aliko. Toba ya Rabi, yuko wapi mtoto huyu? Mungu amsitiri na machafu. Kila siku aliposali, aliomba

> dua, Mungu asiitoe roho yake mpaka pale atakapowatia machoni wanawe (Mohamed, 1980: 106).

Nukuu hiyo inathibitisha kuwa, Waafrika huamini katika uwezo wa Mungu kama sababu mojawapo ya hatima ya maisha ya mwanadamu. Maksuudi anatambua kwamba, hakuna mwanadamu mwenye uwezo wa kuzuia kifo chake, bali ni Mungu pekee. Ndiyo maana anamwomba yeye iliasife mapema. Jambo hili hudhihirisha imani yake kwa Mungu aliyemuumba kuwa ndiye mwamuzi wa mwisho juu ya maisha yake.

**Kifo Husababishwa na Watu**

Mwanadamu huzungukwa na watu mbalimbali katika mazingira yake kama sehemu ya kukamilisha hali ya kutegemeana katika masuala yanayokidhi mahitaji yao. Watu hao wana nafasi kubwa sana katika kuyafanya maisha yake yawe salama au la. Kwa jumla, Waafrika huamini kwamba, hatima ya mwanadamu inaweza kusababishwa na watu mbalimbali wanaomzunguka katika mazingira yake (Mbiti, 1990). Watu hao wanaweza kuwa familia, ndugu, marafiki au majirani ambao daima anaishi na kushirikiana nao katika masuala mbalimbali. Matendo dhahiri au yasiyidhahiri ayafanyayo mwanadamu yanaweza kusababisha hatima ya mwanadamu mwenzake. Katika riwaya ya *Utengano*, mwandishi anabainisha fikra hizi kupitia maelezo ya Biti Kocho ambaye anafafanua ubaya wa Maksuudi uliosababisha hatima ya mkewe wa kwanza Mwanasururu. Cheo chake kilitumika kama fimbo ya kuwachapia wananchi wake, ikiwamo familia yake na kuwadhurumu kadiri alivyotaka. Mwandishi anasema:

> Kwenye meza kulikuwa na picha kubwa ya mwanae, Mwanasururu. Huyu ameshatengana na ulimwengu, amekufa kabla ya siku zake. Na Maksuudi, huyu Maksuudi, ndiye aliyekuwa sababu ya kifo chake. Na ile mali ya mwanae ambayo ilikuwa ikimwezesha yeye Mwanasururu na Farashuu mamaake, yote imefisidiwa na huyu Maksuudi. Nyuma ya machozi haya kulikuwa na picha ya Mwanasururu katika matendo mbalimbali aliyokuwa akiteswa na Maksuudi (Mohamed, 1980: 60).

Katika dondoo hilo tunabaini kuwa mwanadamu anaweza kuwa sababu ya hatima ya maisha ya mwanadamu mwenzake. Kutokana na nguvu na mamlaka aliyokuwanayo Maksuudi, yalisababisha familia na jamii yake kuishi kwa manyanyaso na wengine kukatishwa uhai wao. Huu ni mtazamo wa Waafrika kwa jumla ambapo wanaamini kwamba, matendo fulani ya mwanadamu, huweza kuwa sababu ya hatima ya maisha ya mwingine katika jamii yake. Jambo hili linaendelea kuthibitishwa kupitia maelezo ya kejeli yanayotolewa na Bi. Kazija mkutanoni mbele ya wananchi wenzake. Anaonesha tabia ya Maksuudi jinsi isivyokubalika na jamii nzima kiasi kwamba hafai kabisa kuwa tena kiongozi wa jamii hiyo. Jambo hili linafanyika wakati Maksuudi anajinadi kwa madaha mbele ya wananchi wake ili apewe kura za kuwa

kiongozi katika jamii hiyo kwa awamu nyingine. Mwandishi kupitia kinywa cha Bi. Kazija anasema:

> Maksuudi aliyemwacha mkewe kwa kisa cha kumtorosha mwanawe ati. Na huyu huyu Maksuudi aliyekuwa akimwendea kinyume mkewe. Mbali na mali aliyojilimbikia, nyingine ya unyang'anyi kwa wake zake. Amemnyang'anya mkewe mmoja Mwanasururu, mali yake na mwisho akamwacha na kusababisha kifo chake. Mengi, mengi (Mohamed, 1980:81).

Aidha, Bi. Farashuu anaungana na maelezo ya Bi. Kazija katika kuonesha ubaya aliotendewa mwanawe Mwanasururu kwamba:

> Bi. Farashuu alianza kuyaeleza yote yaliyomkuta mwanawe kwa Bwana Maksuudi mpaka kufikia kumwacha Mwanasururu, kukimbia kwake na kwenda Bobea, kuhunika, kushika mimba, kuingia wazimu na hatimaye kupoteza maisha yake. Na yote hayo sababu ni Bwana Maksuudi. Alihitimisha Bi. Farashuu (Mohamed, 1980: 169).

Kupitia dondoo hiyo, tunabaini kwamba, Maksuudi ameonekana kuwa ni sababu ya kifo cha mkewe Mwanasururu ambapo jamii nzima inaamini na inathibitisha jambo hilo. Jambo hili lipo katika jamii zetu ndiyo maana mwandishi ameona ni vema aoneshe wazi jinsi familia inavyoweza kuwa sababu ya hatima ya maisha ya mwanafamilia mwenzao. Fikra hizi zinaakisi imani ya Waafrika katika kubainisha sababu za kutokea kwahatima ya mwanadamu katika ulimwengu wake halisi.

Pia, Waafrika huamini kwamba, ubaya wa kimaamuzi unaotokana na mitazamo hasi juu ya maisha ya mwanadamu, unaweza kusababisha hatima ya mtu mwingine. Hali hiyo husababishwa na msongo wa mawazo unaomtawala mwanadamu huyo na baadaye kusababisha hatima yake. Jambo hili limebainika katika riwaya ya *Tata za Asumini*, ambapo tunamwona mwandishi anaelezea juu ya hatima ya Asumini ilivyosababishwa na maamuzi ya watu wanaomzunguka katika mazingira yake. Kwa kujiegemeza katika nadharia ya udhaishi, maisha ya duniani yanaonekana hayana maana tena kwa Asumini kutokana changamoto mbalimbali zinazomzingira. Hivyo, anaamua kuandika barua na kuagiza kwamba, apewe Sewa pekee kabla hajajiangamiza. Kilichokuwa ndani yake ni malalamiko kuhusu ubaya aliotendewa na jamii iliyomzunguka kwa jumla, wakiwemo wazazi wake na hatimaye kuishia katika kifo. Maelezo hayo yanasema:

> Waambie, tafadhali waambie Sewa, nimedhurumiwa. Nimedhurumiwa na baba, nimedhurumiwa na mama, nimedhurumiwa na mazingira yaliyonizunguka tokea utotoni, nimedhurumiwa na kila mtu kwa hakika. Hata mimi

> mwenyewe nimejidhurumu kwa namna fulani (Mohamed, 1990: 171).

Asumini anaitazama jamii nzima kama sababu ya kuelekea katika hatima yake kutokana na ubaya walioutenda kulingana na nafasi zao. Watu hao wakiwamo wazazi wake ambao hawakumlea katika hali ya kuweza kuishi kwa kukabiliana na masuala mbalimbali yaliyopo ulimwenguni. Maisha yake tangu utotoni yalikuwa ni ya kitawa ambapo alipokwenda Chuo Kikuu alikuta maisha mengine tofauti na yale aliyoyazoea. Hakupata nafasi ya kuijua kweli kulingana na maisha halisi katika ulimwengu uliozungukwa na watu. Anamtaka Sewa amlee mwanae wa kike kwa kumfunulia yote yaliyopo katika ulimwengu pasipo uficho wa aina yoyote. Suala hili linaonesha wazi kwamba, hatima ya mwanadamu inaweza kusababishwa na mitazamo duni ya watu juu ya dhana ya maisha na maisha yenyewe.

Kwa upande mwingine, mwandishi anaendelea kuthibitisha jambo hili kupitia riwaya ya *Utengano*. Tunamwona mhusika Maimuna anasikitika baada ya kupewa taarifa iliyoletwa na kaka yake Mussa kuhusu kifo cha babake. Anakiri kwamba matendo yake ndiyo yamesababisha hatima ya babake na anaomba asamehewe kwa kuwa hakujua maumivu ambayo baba yake angepata kutokana na kutomsamehe. Anasema:

> "Ba…baba ameshakufa Maimuna"
> "Baba amekufa? Baba amekufa?
> Maimuna alijipapatua mikononi mwa kakaake.
> "Babaangu nisamehe, babaangu nimekuua mimi.
> Basi si kusudi langu, si kusudi langu baba,
> "Alijikamata kichwa akaangua kilio kikubwa zaidi."
> "Nyamaza, Bi Tamima alimnyamazisha mwanawe huku naye milizamu ya machozi ikimpitia" (Mohamed, 1980:175).

Maimuna baada ya kupokea taarifa ya kifo cha babake anajihisi kuwa yeye ndiye msababishaji wa jambo hilo. Hali hii ni kutokana na tabia mbaya aliyoifanya kwa babake ambayo hakupendezwa nayo na kuamua kuishi mbali naye. Kitendo hicho kilimuumiza moyo wake na kusababisha hatima ya maisha yake. Mbali na hayo, mwandishi riwaya ya *Utengano* anaendelea kudhihirisha mtazamo wa Waafrika ya kwamba, Waafrika huamini kuwa, mmoja katika familia anaweza kuwa sababu ya hatima ya wenzake au wazazi wake. Jambo hililinathibitishwa kupitia upweke wa bwana Maksuudi. Mhusika huyu anafikiri kuwa, familia yake ni sababu inayosababisha hatima yake. Pamoja na fikra hizo anataka awatafute popote walipo ili warejee nyumbani na kuishi kama ilivyokuwa zamani. Mwandishi anasema:

> La, la, la la…nitakwenda kuwatafuta wanangu katika uhai wangu uliobaki. Nitawatafuta wao na mama yao warejee kama ilivyokuwa zamani. Nitawatafuta hata kama itakuwa sababu ya kifo changu. Maksuudi alisita ghafla, akautazama mkono wake wa kushoto uliokuwa ukimtetemeka, akajaribu kuuvuta mguu wake, ukamfuata kwa shida….Alielewa kuwa kile sasa kimeshakuwa kilema.

> Aliumia moyoni kuona watoto wake hawapo karibu yake (Mohamed, 1980: 103).

Kimsingi, Maksuudi anajutia suala la kuishi pasipo kuwathamini mke na watoto wake ambapo waliamua kuishi mbali naye. Imekuwa majuto ni mjukuu kwake. Fikra zake zimejiegemeza katika kuwatazama watoto wake kama sababu itakayosababisha hatima ya maisha yake kwa kuwa ana hofu pengine wanaweza kuwa na kisasi juu yake. Kisasi hicho ni kutokana na ubaya aliouonesha kwao na kudhani kwamba nao watakuja kumfanyia ubaya utakaosababisha hatima ya maisha yake.

Kwa namna nyingine, Waafrika huamini katika sihiri kama suala linalosababisha hatima ya maisha ya mwanadamu. Usihiri ni hali ya kufanya uchawi au kuroga watu. Watu wengine wanaamini kwamba mchawi anaweza roga mtu akafa (TUKI, 2014). Kwa kujiegemeza katika nadharia ya udhanaishi, dhana ya maisha na kifo hufafanuliwa kulingana na tajriba za jamii husika. Hivyo basi, tunapoifafanua falsafa ya Waafrika, suala la uchawi linajibainisha kama sehemu ya maisha yao (Makame, 2016). Waafrika wanaamini kwamba, mwanadamu anaweza kutumia nguvu za kisihiri (kichawi) ili kuondoa uhai wa mwanadamu mwenzake. Nguvu hizo zinaweza kubainika kupitia masuala mbalimbali. Baadhi yake ni uwezo wa kumfanya mwanadamu augue ugonjwa ambao hata madaktari hawataweza kupata suluhu ya ugonjwa huo na kupata ajali yenye utata katika utokeaji wake. Pia, nguvu za kisihiri zina uwezo wa kumfanya mwanadamu afe pasipo kuugua. Maana yake ni kwamba, Waafrika wanaitazama nguvu hiyo kwa namna ya kidhanifu, lakini ni sababu mojawapo inayofikiriwa na kuaminiwa katika maisha yao.

Jambo hili linafafanuliwa zaidi na Chuachua (2016) pamoja na Faustine (2017) wanaosema kwamba, fikra za Waafrika zimetawaliwa na suala la uchawi kama kitu chenye kuleta heshima na ufahari katika jamii. Uwezo huu alionao mwanadamu unamfanya aweze kuogopwa na kufanya jambo lolote kwa wengine pasipo kuingiliwa na nguvu za dola kwa kuwa hakuna uthibitisho wa kisayansi unaobainika. Kifo kinapotokea katika mazingira ya Waafrika hata kama kikahusishwa na matukio mengine kama vile kujinyonga, kujiua, ajali au ugonjwa, bado watakihusisha kifo hicho na nguvu za kisihiri. Masuala yanayotawala fikra zao ni kama vilemarehemu amerogwa, ametumiwa pepo au amewekewa kitu kibaya njiani.  Kazi mbalimbali za kifasihi zimedokeza fikra hizi kwa kuwa ni akiso la maisha halisi ya jamii.

Katika riwaya ya *Tata za Asumini*, mwandishi amebainisha fikra hizi kupitiakisa cha kutaka kujiua kwa mhusika mkuu Asumini. Asumini anapiga kelele za kuhitaji kutimiza azima yake ya kujiua akiwa chumbani baada ya kuokolewa na Miriam na Sewa kule bondeni. Kelele hizo ziliwaamsha watu waliokuwa wamelala ambao walichungulia madirisha tukio alilotaka kulifanya Asumini. Kila mmoja alionesha fikra zake juu sababu za Asumini kutaka kufanya hivyo. Kati yao, wapo waliosema kwamba Asumini amerogwa na ndugu zake. Hii inamaanisha kuwa fikra zao

zimejiegemeza katika uchawi na ushirikina kama jambo linaloweza kuhitimisha maisha ya mwanadamu. Mwandishi anaseama:

> Wengine walisema Asumini ana *neurosis* ya mtihani. Wengine walisema Asumini kakataliwa na mwanamme ndiyo maana anataka kujiua. Wengine waliomjua walisema tokea hapo hazimtoshi au karogwa tokea kwao. Na wengine majirani zake walikuja kuuliza kwa imani na kite au kwa umbeya, lakini Miriam bingwa wa kupanga aliwatoa (Mohamed, 1990:9).

Mwandishi kwa kuimulika jamii yake, anaonesha kwamba, hatima ya maisha ya mwanadamu inaweza kusababishwa na kurogwa na wazazi, ndugu au watu wengine wanaomzunguka katika mazingira yake. Suala hili linasawiri fikra za Waafrika ambapo huamini kuwa, nguvu za kisihiri zipo katika maisha yao na zinauwezo wa kuondoa uhai wa mwanadamu. Katika maisha yao, hata ikathibitika kwamba mtu amekufa kwa ugonjwa uliothibitika kisayansi (hospitalini), bado watahusianisha tukio hilo na nguvu za kisihiri. Kinachobainika ni kwamba, imani yao imejigemeza katika kuzimulika nguvu hizokuwa zipo na zinafanya kazi katika maisha yao ya kila siku.

**Kifo Husababishwa na Mwanadamu Mwenyewe**

Waafrika wanaamini kwamba hatima ya mwanadamu inaweza kusababishwa na mwanadamu mwenyewe. Hali hii hutokana na kutenda matendo mbalimbali yanayofungamanishwa na maamuzi yake mwenyewe (Baloyi, 2008). Daima matendo hayo ni hasi kulingana na misingi ya tamaduni husika. Kutokana na ukiushi huo, matendo hayo humrudi mwenyewe na hatimaye kuwa sababu ya kifo chake. Baadhi ya matendo hayo kama vile kufanya dhuluma, uuaji pamoja na uzinzi. Fikra hizo zimebainika katika bunilizi mbalimbali za Kiswahili kupitia matendo ya wahusika wake. Mfano mzuri ni katika riwaya ya *utengano* ambapo tunamwona mhusika Maksuudi anabainisha sababu ya kifo chake kuwa ni ubaya wake mwenyewe. Anasema:

> Usiku ule tuliofika kilabuni alikuwa kama chui mkali. Yule hakuwa mwanangu bali ni shetani. Mimi siponi Mussa, nakufa, na kifo changu kinasababishwa na ubaya wangu mwenyewe, na hasa uchungu wa Maimuna aliyekuwa kipenzi changu. N'nakufa Mussa, lakini mtafute Maimuna umhakikishie kwamba mimi nimempa radhi zangu, na yeye anisamehe (Mohamed, 1980:175).

Maksuudi anakiri wazi kuwa matendo yake ndiyo yanayosababisha kifo chake. Hakika, Maksuudi hakuitendea haki familia na jamii yake kwa jumla. Aliwanyanyasa na kuwafukuza nyumbani familia yake pasipo kufikiri kwamba atakapofikwa na tatizo lolote lile atakosa mtu wa kumsaidia. Ndivyo ilivyokuwa baada ya kupata maradhi ya mara kwa mara hakuwa na msaada kwa kuwa familia

yake ilikuwa mbali naye. Kwake ikawa ni majuto yasiyoelezeka ambapo mpaka anataka kufa hajaiona familia yake akiwamo mwanae mpenzi Maimuna. Kwa kujikita katika mwegamo wa nadharia ya udhanaishi, Maksuudi anayatathmini mapito na maisha yake yenye kujaa fedheha, mashaka hofu kuwa hayana maana tena. Jambo hili linaonesha jinsi Waafrika wanavyoamini kuwa matendo mabaya ayatendayo mwanadamu ni sababu mojawapo ya hatima yake.

Suala hili linathibitika tena katika riwaya ya *Tata za Asumuni* ambapo tunamwona Asumini anataka kujiua kwa sababu ya maamuzi yake mwenyewe. Pamoja na malezi aliyoyapata, bado maamuzi yake juu ya namna ya kuishi ndiyo ilikuwa sababu ya kujiangamiza kwake. Maamuzi hayo yalianzia katika suala la kuachamasomona kujiingiza katika starehe iliyosababisha kadhia na misukosuko mingi na hatimaye kutaka kujiua mwenyewe kama suluhisho la jambo hilo. Haya yanabainika pale anapokiri mwenyewe katika barua aliyomwandikia mpenzi wake Sewa ambapo anasema "Hata mimi mwenyewe nimejidhurumu kwa namna fulani" (uk.171). Mwandishi ameibua na kuonesha suala hili kwa kuwa ni sehemu ya maisha ya wanadamu katika mazingira yao halisi. Pia, maelezo ya Sewa nayo yanatudhihirishia fikra hizi ambapo anaonesha kutoamini kama Asumini anaweza kujihukumu na kujidhuru mwenyewe. Mwandishi anasema kwamba: "Asumini hakuonekana. Sewa hakuamini kwamba angeweza kupotea kabisa kabisa.Hakuamini wala hakutaka kuamini kwamba angeweza kujidhuru" (uk. 172). Kwa jumla, Asumini alikata tamaa na kuyaona maisha hayana maana kwake hivyo, ni vema ajisababishie kifo. Hii ni dhahiri kwamba Waafrika katika kuzitazama sababu za hatima yao, wanajiegemeza katika misingi inayoaminiwa kuwa ni kweli kulingana na maisha yao halisi.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili kuhusu sababu mbalimbali za hatima ya maisha ya mwanadamu kulingana na mitazamo ya Waafrika kwa kujiegemeza katika kibunilizi za Kiswahili. Data zilizofafanuliwa zimetokana na usomaji wa maandiko mbalimbali. Maandiko ya msingi ya data hizo ni riwaya za *Utengano*na *Tata za Asumini* zilizoandikwa na mwandishi Said Mohamed. Riwaya hizi zimesukwa kwa kujiegemeza katika misingi ya maisha ya jamii inayomzunguka mwandishi ambayo ni sehemu ya Waafrika. Ameonesha maarifa mbalimbali ya kifalsafa yanayodhihirisha ukweli wa jamii kulingana na tamaduni zao. Matokeo yanaonesha kwamba, riwaya hizi imesheheni masuala mbalimbali muhimu yanayosawiri fikra za Waafrika kwa jumla. Moja ya mausala hayo ni suala la fikra za Waafrika kuhusu kuwapo kwa sababu zinazosababisha hatima maisha ya mwanadamu kulingana na tamaduni zao. Baadhi ya masuala yaliyofafanuliwa katika mjadala wa makala hii ni kifo husababishwa na maamuzi ya Mungu, ubaya au uovu aufanyao mwanadamu mwenyewe katika maisha yake na watu wanaokuzunguka mathalani, ndugu, marafiki na majirani.

**Marejeo**

Baloyi, L. (2008). *The African Conception on Death: A Cultural Implication*. South Africa: University of South Africa.

Camus, A. (1955). *The Myth of Sisyphus and Other Essay*. London: Vintage Books.

Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Duwe, M. (2016). Mdhihiriko wa Falsafa ya Uduara katika Sanaa za Maonesho za Jamii ya Wangoni. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Faustine, S. (2017). Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Godin, A. (1972). *Death and Presence: The Pyschology of Death and the After Life*. Brussels: Lumei Vitae Press.

Idowu, E. B. (1973). *African Traditional Religion*. New York: Obis Books.

Makame, S. F. (2016). Matumizi ya Falsafa ya Usihiri katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mbiti, J. S. (1990). *African religions and philosophies*. United Kingdom: Heineman Educational.

Murphy, G. L. (2003). *African-American Faith in America*. New York: Oxford University Press.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma Tanzania: Central Tanganyika Press.

Mohamed,S. A. (1980). *Utengano*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.

Mohamed, S. A. (1990). *Hadithi za Kusisimua: Tata za Asumini*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Ltd.

Shields, J. M. (2008). *An Eschatological Imagination: A Revisionist Christian Eschatology in the Light of David Tracy's Theological Project*. New York: Peter Lang Publishing.

Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi; kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza Tanzania: Serengeti Bookshop.

Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswhili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wafula, R., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakika wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Open University Press.

Wamitila, K. W. (2016). *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. New Delhi: Vile-Muwa Publishers Ltd.